WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IFUNDA

S. L. P 7 IFUNDA

29/05/2020

KUMB.NA.**IGHS/ S.1806/ADM/2020/Joi/VOL.09**

Simu: Mkuu wa shule 0714682501, Makamu 0752683122.

Mzazi/mlezi wa Mwanafunzi……

S.L.P……..

YAH:MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA HALMASHAURI YA IRINGA, MKOA WA IRINGA MWAKA 2020/2021.

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na **Kidato cha Tano** katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ifunda mwaka **2020/2021, kati ya Tahasusi zifuatazo PCB /PCM/PGM/CBG/EGM/HGE NA HGK.**

Mahali ilipo shule

Shule ya wasichana ya Ifunda ipo umbali wa kilometa 43 kusini mwa Manispaa ya Iringa, usafiri wa basi kutoka Mjini Iringa unapatikana katika kituo cha mabasi Iringa mjini nauli ni Tsh 1,500/= shuka kituo kinachoitwa **IFUNDA SHULE.**

Muhula wa masomo utaanza tarehe …….. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……. na mwisho wa kuripoti utatangazwa na Serikali. Muda wa kupokea wanafunzi mwisho saa kumi na mbili jioni(12.00)

Mambo ya kuzingatia : SARE YA SHULE

A: Wakati wa Masomo darasani na atokapo nje ya shule

Mchoro wa sketi zote, darasani(brauni) na shamba dress(orange)



1. Sketi mbili za brauni zenye Rinda box(marinda mawili) kitambaa cha suti, iwe na urefu mpaka chini miguuni, ili kuepuka kutofautiana kwa rangi njoo ushone huku huku ifunda .
2. Mashati meupe mawili yenye mikono mirefu anunue mwenyewe.
3. Viatu vyeusi visivyo na kisigino kirefu wala urembo wowote,aje navyo
4. Soksi nyeupe zisizo na urembo, aje nazo

   NB: wasichana wa kiislamu wanaruhusiwa kuvaa hijabu kama ifuatavyo

   1. Sketi ndefu mpaka chini miguuni, rangi ya brauni kitambaa cha suti ,iwe na urefu mpaka chini miguuni ili kuepusha kutofautiana njoo ushone huku ifunda.
   2. Nusu kanzu nyeupe mikono mirefu aje nayo
   3. Kijuba/mtando mweupe usio na urembo aje nao

B:wakati wa kazi na mapumziko(au kazi za nje)

1.sketi za orange(machungwa) rinda box kitambaa cha suti shona mwenyewe kama unaijua rangi iwe ndefu mpaka chini miguuni.

2. T-shirt Nyeupe isiyo na maandishi, yenye Kola aje nayo ili iwekwe maandishi ya shule.

C: wakati wa michezo

1. Fulana (T-shirt) nyeupe isiyo na maandishi aje nayo

2. Bukta ya blue na minisketi ya blue aje nayo

3. Raba za michezo anunue mwenyewe

4. Track suit nyeusi ya adidas yenye michirizi mieupe pembeni aje nayo isiwe na kofia.

5. Sweta rangi ya kijani jeshi aje nayo kama anajua rangi vema kama hujui rangi utanunua Iringa

6. Aje na Kikoi cha kimasai Rangi Nyekundu chenye draft ndogo sana. na Mzura mwekundu kwa ajili ya baridi

7. Pull neck Nyeupe mbili aje nazo kwa ajili ya Baridi.

D:Vifaa vya Bwenini

1. Kila mwanafunzi aje na godoro futi $2\frac{1}{2}$ X 6
2. Blanketi 1 zito,shuka mbili rangi ya pinki ,mto na foronya rangi ya pinki
3. Ndoo,kandambili,kanga,au kitenge(kwa matimizi ya bwenini tu na siyo nje ya bweni
4. Mwavuli,sahani,bakuli,kijiko,mswaki na kikombe
5. Chandarua kwa ajili ya mbu aje nacho

E:Vifaa vya masomo

1. Madaftari Madogo 10 kwa ajili ya Test za kila wiki, na Counterbook Q3/Q4 si chini 6
2. Vitabu vya tahasusi husika kwa mwanafunzi na Bando 1(moja tu). la Karatasi zenye mstari (Ruled paper)
3. Kalamu, mkebe na scientific calculator(non- programmable) kwa masomo ya sayansi na hesabu

4. Kila mwanafunzi alete rim moja ya A4 kwa ajili ya mitihani ya Mhula na graph pad, bando moja.
5. Copy ya result slip ya kidato cha nne aje nayo
6. Cheti cha kuzaliwa (birth certificate) ni muhimu aje nacho
7. Picha za passport size za wazazi/walezi zitawekwa kwenye faili la mwanafunzi.

F: **Vifaa vya Usafi:**(Aje na vifaa kulingana na Tahasusi (comb) aliyochaguliwa, yaani moja kati ya hizi zifuatazo;-

1. Squizer (brushi ya kukaushia maji 1 na chelewa 1. (PCM),
2. Brush .1 ya kusugulia sinki la choo, Fagio chelewa 1. mbili na squizer 1 ya kukaushia maji ndani **(PGM**),,
3. Soft bloom 1na chelewa 1.Brush ya kusugua sink la choo. 1 **(EGM**),,
4. Jembe jipya moja lililonolewa na mpini wake na chelewa moja. **(PCB),**
5. Hard bloom 1. na Squizer 1 na chelewa 1. **(CBG),,**
6. Mkasi mmoja wa kukatia maua na chelewa 1.**(HGE)**.
7. Reki yenye mpini wa chuma ya kukusanyia taka na chelewa 1. (**HGK)**

G: A**da na michango:**

1. Ada ya shule ni Tshs. **70,000/-** kwa mwaka au Tshs. **35,000/-** kwa muhula. Lipia tawi lolote nchini Bank ya **NMB** katika akaunti hii **60501100110**. Jina la akaunti ni **IFUNDA GIRLS SEC. SCHOOL**. Kisha uje na **Pay-in-slip** iandikwe jina la mwanafunzi na kidato, mwanafunzi aje nayo shuleni anapokuja kuripoti. (**Fedha taslimu hazitapokelewa**) **Mwanafunzi hatapokelewa bila risiti ya ada.**
2. **Michango ya ifuatayo itawekwa kwenye account iliyopo hapo juu no.1.**
   a. Tahadhari …….. 5,000/-
   b. Kitambulisho …….. 5,000/-
   c. Matibabu…….. 10,000/-
   d. Taaluma …….. 20,000/-
   e. Ukarabati …….. 15,000/-
   f. Mlinzi/wapishi/vibarua …….. 30,000/-
   g. Nembo Kwenye T-shirt …….. 2,000/-
   h. Mafuta ya gari ……..5,000/-
   i. Umeme……..10,000/-
   j. Maandishi kwenye T-shirt ……..4,000/-

JUMLA YA MICHANGO NI: 106,000/= Ukijumlisha na ada 70,000/-(kwa mwaka), JUMLA KUU TSH 176, 000.00

MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo darasani/utoro
iii. Kudharau bendera ya Taifa
iv. Kugoma na kuhamasisha mgomo
v. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake , walimu, walezi na jamii kwa ujumla
vi. Kupigana kwa mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu, mtumishi au mtu yeyote yule

vii. **Kusuka nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni**

viii. **Uvutaji sigara, Ulevi,unywaji pombe au kutumia madawa ya kulevya**

ix. **Uvutaji wa sigara**

x. **Uasherati, uhusiano wa kimapenzi, kuoa au kuolewa**

xi. **Kuwa na ujauzito au kutoa mimba**

xii. **Kushiriki uhalifu, siasa, na matendo yoyote yale yanavunja sheria za nchi**

xiii. **Kutembelea majumba ya starehe.**

xiv. **Kufanya jaribio lolote la kutaka kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu**

xv. **Uhalibifu wa mali ya umma kwa makusudi.**

N:B.Bodi illifikia uamuzi kuwa, adhabu ya kukutwa/kutumia simu shuleni ni Tofali ndogo 3500 zilizochomwa kwa ajili ya kujenga wigo wa shule wa ukuta na Bulb tronic 20, Volt 40. kwa ajili ya ulinzi usiku kwa wanaotoroka.

Mambo Mengine Muhimu ya kuzingatia kwa Mwanafunzi awapo shuleni

1. Mwanafunzi hataruhusiwa kuwa nje ya shule ila kwa ruhusa maalumu ya Mkuu wa shule, na atatakiwa kurudi shuleni kabla ya sa 10:00 jioni. Tena ni marufuku kwa mwanafunzi kutembea peke yake akiwa nje ya shule ni lazima watembee kwa makundi kuanzia wawili,watatu n.k
2. Shule hii ni ya serikali kila mwanafunzi atambue kuwa akiwa shuleni hatakuwa tofauti Na mwenzie kwa msingi ya kidini, kikabila na Kiuchumi.
3. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kujadili dini au siasa ya mwingine, wala hairuhusiwi kuwa na mjadala ya kidini au siasa hapa shuleni, kwani shule haina kanisa wala msikiti, ukiukwaji wa maelezo haya yatasababisha mwanafunzi kuondolewa shuleni.
4. Katika siku za ibada(Ijumaa,Iumamosi na Jumapili) wataambatana na walezi wao kwenda katika nyumba za ibada zilizopo ndani ya kijiji cha Ifunda tu.
5. Wanafunzi wote wanapaswa kuvaa sare ya shule wanapotoka nje ya shule. Nguo yoyote hairuhusiwi. Aidha pasiwepo na mwanafunzi kutoka darasani na kwenda Ibadani muda wa vipindi vya darasani, kwani vipindi vya dini vipo kila wiki kwa dini zote, hivi vipindi vinatumika kuwafundisha wanafunzi maadili ya Imani zao na siyo vinginevyo.
6. Ratiba ya masomo hairuhusu mwanafunzi kutoka kwenda kambi za kidini, kongamano za kidini au kufanya shughuli ya kidini wakati shule inaendelea. Walimu wa madhehebu yote tunaomba mafundisho yote ya dini yafanyike muda wa vipindi vyao vya dini na siku za ibada,pasiwepo na mwingiliano wa aina yoyote na ratiba za shule.
7. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuchelewa tarehe ya kufungua shule, akichelewa hata kwa siku moja tu, atarudishwa nyumbani ili aje na mzazi/mlezi wake halali ili tujue kama alikuwa mahali salama.
   pia Kuingia shuleni Mwisho saa 12.00 jioni, akichelewa walinzi watafunga geti hatapokelewa. pia akifika shule hairuhusiwi kuingia au kutoka nje ya shule kupitia kwenye wigo /fensi bali apite getini.

NB: tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa shule……

Jina la Mkuu wa shule……..

Mhuri wa Mkuu wa shule……

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
SEKONDARI YA WASICHANA IFUNDA
FOMU YA KUKUBALI NAFASI

A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI (Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)

Jina kamili (kama kwenye results slip) …….. Tarehe ya Kuzaliwa ……. Kabila …….. dini na dhehebu …….. COMB niliyochaguliwa …….. Mwaka wa masomo …… shule nitokayo …….. Mahali niishipo …….. mkoa …… anwani ……..

Jina la baba/mlezi …… kazi yake ……..

Jina la mama/mlezi …….. kazi yake ……..

Wazazi/walezi wanaishi (wapi)…….. pamoja/wametengana ……..

Anwani ya mzazi/mlezi …… simu ……

Wakati wa likizo nitakuwa kwa (mtaje) …… wapi ……..

Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi:

Sahihi ya mwanafunzi …… tarehe …….

KUKUBALI NAFASI (mwanafunzi mwenyewe ajaze)

Mimi …….. nimesoma maagizo kwa makini na kuzielewa taratibu za shule na nipo tayari kuzifuata. Hivyo ninakubali nafasi niliyopewa na nitafika shuleni tarehe iliyopangwa.

B: IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

Mimi …….. ambaye ni …….. Wa mwanafunzi huyu nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na sheria za shule katika Fomu ya Kujiunga. Nipo tayari ajiunge na shule hii, ninaahidi kumtolea ada, michango na mahitaji yote ili aweze kupata elimu yake vizuri katika shule hii. Aidha nitasaidiana na walezi wa shuleni katika kumlea mwanafunzi huyu katika maadili mema na kuitika wito wa kufika shuleni pale nitakapohitajika.

Anuani yangu ya kudumu …….. simu ……

Nikipata uhamisho ama kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi. Ndugu zangu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi akiwa shuleni siku za wageni ni:-

1. …… uhusiano kwa mwanafunzi …….. Simu ……..
2. …… uhusiano kwa mwanafunzi …….. Simu ……..
3. …… uhusiano kwa mwanafunzi ……..simu ……..

Nathibitisha Taarifa nilizotoa ni sahihi na kweli: Sahihi ya mzazi/mlezi …….. Tarehe ……..

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY
IFUNDA GIRLS HIGH SCHOOL
STUDENT'S MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmistress of Ifunda Girls High School, P. O. Box 7 Ifunda.

To Medical officer

……

……

……

RE: STUDENT NAMED …….. FORM ……. COMB ……. AGE ……. SEX ……

Please, examine the student mentioned above and comment on her health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either Yes or No as you find appropriate. Thank you in advance!



SALINGWA Z.
HEADMISTRESS

Do the student have problem in connection with

- Sight? **Yes / No** If yes state ……
- Hearing? **Yes / No** If yes state ……
- Speech? **Yes / No** If yes state ……
- TB? **Yes / No** If yes state ……
- Blood Pressure? **Yes / No** If yes state ……
- Any Physical disability? **Yes / No** If yes state ……

Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this school? **Yes / No**
If no please state the reasons ……
Name of Medical Officer …….. signature ……..
Designation & Stamp ……. Date ……